**Kikao cha Pili—Tarehe 7 Novemba, 1975**

*(Mkutano ulianza saa kumi jioni)*

## DUA

*Nd. Spika (Mtwa Adam Sapi Mkwawa) alisoma Dua*

## KIAPO CHA UAMINIFU

*Nd. Titus Ambrose Mpanduji aliapa kiapo cha uaminifu na kukaa katika nafasi yake katika Bunge.*

## UCHAGUZI WA WABUNGE WA TAIFA WA MIKOA

Mkoa wa Dodoma.
Mkoa wa Morogoro.
Mkoa wa Mwanza.
Mkoa wa Pwani.
Mkoa wa Rukwa.
Mkoa wa Ruvuma.
Mkoa wa Shinyanga.
Mkoa wa Singida.
Mkoa wa Tabora.
Mkoa wa Tanga.
Mkoa wa Ziwa Magharibi.

*(Nd. Wabunge waligawiwa karatasi za kila Mkoa kwa wakati wake na kupiga kura).*

## UCHAGUZI WA WABUNGE WA TAIFA WALIOPENDEKEZWA NA MASHIRIKA

**Spika:** Nd. Wabunge mtagawiwa karatasi kama hii. *(Hapa Wabunge walionyeshwa mfano wa karatasi ya uchaguzi)* Katika uchaguzi wa Wabunge wa Taifa na karatasi hii ina majina ishirini na tisa. Kwa hiyo katika majina ishirini na tisa kinachotakiwa ni kutia vema upande huu ulipoandikwa kura, vema kumi na tano. Ukiongeza zikawa kumi na sita basi karatasi yako ya kura itakuwa imeharibika.

*(Hapa Nd. Wabunge waligawiwa karatasi za kura na kupiga kura zao).*

## UCHAGUZI WA WAJUMBE WA BARAZA LA KUTUNGA SHERIA LA AFRIKA MASHARIKI

**Spika:** Nd. Wabunge utaratibu ni kama ule wa uchaguzi wa Wabunge wa Taifa. Sasa mtawapigia kura Wabunge wa Afrika Mashariki. Na orodha hii ina majina kumi na saba, unachotakiwa ni kuwapigia kura tisa. Usipotaka hata kuwapigia tisa ni sawa, juu yako. Lakini wasiwe zaidi ya tisa, ikiwa utazidisha idadi basi utakuwa umeharibu karatasi yako ya uchaguzi.

Ndugu Wabunge, sasa natangaza majina ya Ndugu watakaosimamia kuhesabu kura za Wagombea Mikoa, Taifa na Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki.

Mkoa wa Dodoma ni Nd. Kingwaba Hassan Kingwaba na Nd. Ngalai.

Mkoa wa Morogoro: Nd. Nkurlu na Nd. Wambura.

Mkoa wa Mwanza: Nd. Rashid Abdallah na Nd. Mujengi Gwao.

Mkoa wa Pwani: Muhsin bin Ali na Nd. Ibrahim Kajembo.

Mkoa wa Rukwa: Nd. Said Ali Bungara na Nd. Edgar Majogo.

Mkoa wa Ruvuma: Nd. Ayub Kimbao na Nd. Juma Makame.

Mkoa wa Shinyanga: Nd. Herman Kirigini na Nd. Mohamed Mfaume.

Mkoa wa Singida: Nd. Richard Mazengo na Nd. Felix Mwanambilimbi.

Mkoa wa Tabora: Nd. Chediel Mgonja na Nd. Amiri Jamal.

Mkoa wa Tanga: Nd. Godfrey Mugissa na Nd. Maalim Nabahan.

Mkoa wa Ziwa Magharibi: Nd. Tobi Mweri na Nd. Albert Nachunga.

Watakaosimamia kura za viti vya Wabunge wa Taifa ni:—

Nd. Kindasi Hoza, Nd. Joseph Macha, Nd. Kingunge Ngombale-Mwiru; Nd. Said Washoto, na Nd. Hadija Swedi.

Watakaosimamia kura za viti vya Afrika Mashariki ni:—

Nd. Tabitha Siwale, Nd. Ali Mwinyigogo, Nd. Alphonce Rulegura, Nd. Hussein Shekilango na Nd. Samuel John Sitta.

Kwa hiyo Nd. Wabunge ninaliahirisha Bunge kwa muda ili kuwapa nafasi Ndugu hao wakahesabu kura hizo, na mara tu watakapokuwa tayari tutapiga tena kengele kusudi turudi. Ikiwa kengele bahati mbaya imeharibika, basi tutapiga mayowe. *(Kicheko.)*

Kwa hiyo Nd. Wabunge, ninaliahirisha Bunge kwa muda.

*(Saa 11.47 Bunge liliahirishwa kwa muda)*
*(Saa 1.50 jioni Bunge lilirudia)*

**Nd. Spika:** Ninamwomba Nd. R. M. Kawawa ikiwa kama Makamu wa Rais wa Chama cha TANU atoe hoja kwamba tuendelee na shughuli kwa vile saa ambayo tunaahirisha Bunge bado dakika chache tu.

**Makamu wa Rais wa Chama cha TANU:** Nd. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge liendelee kukaa mpaka tumemaliza shughuli ya leo.

**Nd. Mwakawago:** Nd. Spika, Naafiki.

**Nd. Spika:** Nd. Wabunge, sasa tutahitajiwa kupiga kura tena. Mkoa wa Ruvuma, Nd. Paul Joseph Mhaiki na Nd. Zaitun Fadhili Selemani kwa sababu kura zao zilikuwa karibu karibu tutapiga kura tena. Halafu Mkoa wa Singida, Nd. Zephania Mwanja na Nd. Anna Asher Namilikwa itabidi tuwapigie kura kwa sababu kura zao zimekuwa karibu karibu. Mkoa wa Tabora Nd. Julius Amon Massongo na Nd. Mosi Ramadhani (Bi. Tambwe).

*(Uchaguzi ulirudiwa na kura zilipigwa kwa Mikoa ya Ruvuma, Tabora na Singida).*

**Nd. Kintu:** Nd. Spika, kuna kura ambazo tumepiga sasa hivi zimechanganyika. Wengine tumepiga za Singida, wengine tumepiga za Tabora. Sasa, hatujui zipi tunapiga sasa. Mimi nimepiga Singida, sanduku lililopita ni la Tabora na nilipouliza wakasema zinapigwa za Tabora.

**Makamu wa Rais wa Chama cha TANU:** Nd. Spika, nadhani kura zilizogawiwa ni za Singida, lakini kwa bahati mbaya sanduku lililokusanya kura hizo ni la Tabora. Kwa hiyo—ndiyo ninachosema hicho. Kura tulizopiga ni za Singida, ama sivyo?. Lakini kwa bahati mbaya sanduku lililokusanyia kura yenyewe ni la Tabora. Sasa sielewi kama kuna jamaa amepiga kura ya Tabora. Karatasi bado za Singida. Hazijaenea. Za Singida tayari ndiyo zenyewe hizo. Tumepiga kura za Singida na sanduku lililokusanyiwa ni la Tabora. Sasa walikuwa wanabadilisha tu hapa. Walikuwa wanabadilisha tu masanduku. Ndilo jambo lililofanyika sasa hivi.

**Mjumbe Fulani:** Nd. Spika, mimi nimepewa karatasi ya Tabora ambayo bado sijaitumbukiza katika sanduku.

**Nd. Spika:** Leta, watakupa nyingine.

**Mbunge Fulani:** Ndiyo kusema kwamba karatasi za Singida sijapata.

**Nd. Spika:** Basi uje upate.

**Nd. Songambele:** Nd. Spika, tungeomba maelezo mazuri zaidi. Kwanza nianze kura za kwanza tumepiga za Ruvuma, pili kwa sisi wengine tumepiga ya Tabora na Singida hatujapata sisi sasa hivi. Sasa tunataka tupate maelezo vizuri maana yake tumepiga ya Ruvuma na tumepiga ya Tabora.

**Nd. Spika:** Ya Tabora bado.

**Nd. Songambele:** Tumepiga, Nd. Spika.

**Makamu wa Rais wa Chama cha TANU:** Nd. Spika, nadhani wakati tunagawa makaratasi wanatangaza "Sasa ni Singida" "Sasa ni Ruvuma". Kwa hiyo kama umepewa nyingine sema hii siyo pale pale. Maana tunapiga kura kwa majimbo. Tumepiga Ruvuma, sasa ilikuwa zamu ya Singida. Kama ulipewa karatasi ya Tabora ni makosa hayo. Ingebidi uone. Kwa hiyo, hiyo kura yako imeharibika.

**Nd. Siyovelwa:** Nd. Spika, kwa maelezo yaliyotolewa katika Baraza letu kila mtu alielewa na kila tunapoanza kura moja inatamkwa wazi wazi tunapiga kura ya Singida, halafu inatamkwa tena baadaye tunapiga kura ya Mwanza. Kila mtu anasikia hapa. Yo yote yule anayepewa karatasi isyokuwa na tamko la Kiti anapigaje kura hiyo? Tungemtazamia huyo atarudisha karatasi yake. *(Makofi.)* Wala haina ugomvi ila ina nafasi ya kupoteza wakati tu. Sasa tumesema waliopiga kura zingine zile zote walijua wanapiga nini. Na warudishe. Tulipiga kura hii iliyotangazwa basi na tuendelee na hiyo.

**Nd. Spika:** Nd. Wabunge wasimamizi wa kuhesabu kura ni kama ifuatavyo:—

Mkoa wa Ruvuma: Ameteuliwa Nd. Venant Joseph Lwabuti na Nd. Stephen Salimu Nandonde.

Mkoa wa Singida: Ameteuliwa Nd. Geoffrey Oscar Mhagama na Nd. Abel Kyagunya Mwanga.

Mkoa wa Tabora: Ameteuliwa Nd. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya na Nd. Blasio Katura Sizimwe.

Sasa kabla sijasimamisha Bunge wakati kura zikihesabiwa ningependa tu kuchukua nafasi hii kuwaomba wale Nd. Wabunge ambao watafanikiwa na matokeo ya uchaguzi huu waende nje mara upande huo kusudi wakutane na watu wa magazeti wawapige picha. Sasa Nd. Wabunge nalisimamisha Bunge hili kusudi Ndugu wapate kuhesabu kura halafu baadaye nitawaita tena kusudi niwasomee matokeo. Ahsante.

*(Saa 2.15 Bunge lilifungwa)*

*(Saa 3 kamili Bunge lilirudia)*

## MATOKEO YA UCHAGUZI WABUNGE WA TAIFA WA MIKOA

**Nd. Spika:** Matokeo ya Uchaguzi:

Mkoa wa Dar es Salaam amechaguliwa Nd. Peter Macha.

Mkoa wa Dodoma amechaguliwa Nd. Stephen Philip Assey.

Mkoa wa Iringa amechaguliwa Nd. I. M. Kaduma.

Mkoa wa Kigoma amechaguliwa Nd. Leonard Manwa Kaboboye.

Mkoa wa Kilimanjaro amechaguliwa Nd. Abdallahman R. Msangi.

Mkoa wa Lindi amechaguliwa Nd. John Michael Aidi.

Mkoa wa Mara amechaguliwa Nd. Joseph Kizurira Nyerere.

Mkoa wa Mbeya amechaguliwa Nd. Jackson Wilfred Mwakibwili.

Mkoa wa Morogoro amechaguliwa Nd. Yona Francis Mgonde.

Mkoa wa Mtwara amechaguliwa Nd. Robert Ng'itu.

Mkoa wa Mwanza amechaguliwa Nd. Corona Faida Busongo.

Mkoa wa Pwani amechaguliwa Nd. Kasmiri Yohana Komba.

Mkoa wa Rukwa amechaguliwa Nd. Francis X. Itala.

Mkoa wa Ruvuma amechaguliwa Nd. Zaituni Fadhili Selemani.

Mkoa wa Shinyanga amechaguliwa Nd. Said S. Ng'wanang'walu.

Mkoa wa Singida amechaguliwa Nd. Ana Asher Namilika.

Mkoa wa Tabora amechaguliwa Nd. Mosi Ramadhan (Bibi Tambwe).

Mkoa wa Tanga amechaguliwa Nd. Yahaya Bakari Lukoya.

Mkoa wa Ziwa Magharibi amechaguliwa Nd. Edward Barugira Muyagi Barongo.

## WABUNGE WA TAIFA

Amechaguliwa Nd. Ismail Salehe Ismail.
Amechaguliwa Nd. Dk. Leader Stirling.
Amechaguliwa Nd. Philip G. Ndaki.
Amechaguliwa Nd. Arnold J. Temu.
Amechaguliwa Nd. Mboni O. Cheka.
Amechaguliwa Nd. Margaret J. Chogo.
Amechaguliwa Nd. Emmanuel B. Kibira.
Amechaguliwa Nd. Hindu B. Lilla.
Amechaguliwa Nd. Nicholas A. Kuhanga.
Amechaguliwa Nd. Crispin Tungaraza.
Amechaguliwa Nd. Ezekiel M. Waryuba.
Amechaguliwa Nd. Venance F. Ngula.
Amechaguliwa Nd. Mary E. Hancock.
Amechaguliwa Nd. Anne S. Makinda.
Amechaguliwa Nd. Henry O. Clemens.

## WAJUMBE WA BARAZA LA KUTUNGA SHERIA LA AFRIKA MASHARIKI

**Nd. Spika:** Wafuatao wamechaguliwa kuwa Wajumbe katika Bunge la Afrika Mashariki:—

Nd. Joseph Kizurira Nyerere.
Nd. Usi Haji.
Nd. Benjamin Mkapa.
Nd. Daniel A. N. Yona.
Nd. Simon Michael M. Mbilinyi.
Nd. Lucy Selina Lameck.
Nd. Kassim M. M. Guruli.
Nd. Gabriel E. Kagaruki.
Nd. Getrude Ibengwe Mongella.

## KUAHIRISHA BUNGE

**Makamu wa Rais wa Chama cha TANU:** Nd. Spika, natumaini Nd. Wabungew amekwishaandika hayo majina yote ya Ndugu zetu ambao tumewachagua. Nataka kutoa pongezi kubwa sana kwa kazi kubwa ambayo tumeifanya leo ambayo ni *record* kusema kweli, tumeifanya vizuri sana na tulikubali kukaa mpaka saa hizi lakini siku ya kupongezana na kuagana ni kesho. Na sikusudii kutoa pongezi zo zote leo lakini Nd. Spika,—Lo, furaha zimezidi sana—Nd. Spika, matokeo ya jana ya uchaguzi wa Spika, kidogo Ndugu zetu wa magazeti na Radio wamepotosha. (*Makofi.*) Na ningewaomba kwa faida ya mmoja wetu ndani ya Bunge hili wasahihishe vile walivyotangaza. (*Makofi.*) Katika kikao chetu cha TANU na *Afro-Shirazi Party* tulikubaliana mgombeaji Kiti cha Spika atakuwa nani, ni huyo tu mmoja na Bunge lilikuwa ni kuthibitisha uamuzi wetu wa kikao cha TANU na *Afro-Shirazi Party*. (*Makofi.*) Nd. Mang'enya hakusimama wala hakusimamishwa kugombea kiti cha Spika. (*Makofi.*) Kwa hiyo yule ambaye alimpigia kura kusema kweli kura yake ingestahili ihesabiwe kwamba imeharibika. (*Makofi.*) Lakini kwa sababu ya Kanuni zetu za Bunge bado ni za kizamani, nadhani ni jambo ambalo ingefaa liangaliwe ili tusije tukaaibika tena safari ijayo. Kanuni hiyo ndiyo pengine imempotosha mwenzetu mmoja akamtaja Mbunge au mwenzetu mmoja ambaye hatukukubaliana kwamba agombee kiti cha Spika.

Sasa ningeomba watuelezee Taifa lielewe kwamba Nd. *Chief* Erasto Mang'enya yeye hakugombea kiti cha Spika. (*Makofi.*) Ile kura ilipotoka tu na ilikubalika kuwa iwe kura kwa sababu ya Kanuni zetu za kizamani.

Baada ya hayo, Nd. Spika, tunakusudia kesho asubuhi baada ya Dua yetu tutawaapisha hawa Ndugu zetu—watakuja kuapa hapa wale ambao wamepita katika uchaguzi wa Bunge letu hili. Na baada ya hapo tutakuwa tumemaliza rasmi Kikao chetu safari hii, zitabaki hotuba chache za kuagana na kupongezana maana itakuwa hapo kesho ndipo Bunge letu litakuwa limekamilika rasmi. Sasa baada ya hayo naomba tu kuwakumbusha Nd. Wabunge kwamba kesho saa tisa tutakutana tena katika Ofisi ya Bunge katika Kikao cha TANU na *Afro-Shirazi Party* kwa mujibu wa kukutana na Rais wetu. Na jioni saa 12 wote Nd. Wabunge, wa Bunge hili lote tutakaokutanika kesho, wote tunakaribishwa Ikulu saa 12. (*Makofi.*) Tunakaribishwa na Nd. Rais.

Baada ya hayo naomba kutoa hoja kwamba Bunge liahirishwe mpaka kesho asubuhi saa tatu.

**Nd. Dk. Chagula:** Naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

*Bunge liliahirishwa saa 3.16 usiku mpaka Jumamosi tarehe 8 Novemba, 1975 saa 3.00 asubuhi.*

**Kikao cha Tatu—Tarehe 8 Novemba, 1975**

*Mkutano ulianza saa tatu asubuhi)*

## DUA

*Nd. Spika (Mtwa Adam Sapi) alisoma Doa.*

## KIAPO CHA UAMINIFU

*Wabunge wafuatao waliapa kiapo cha uaminifu na kuchukua nafasi zao katika Bunge:—*

Nd. John Michael Aidi.
Nd. Stephen Philip Assey.
Nd. Edward Barugira Muyagi Barongo.
Nd. Corona Faida Busongo.
Nd. Mboni Omari Cheka.
Nd. Margaret Chogo.
Nd. Henry Orauya Clemens.
Nd. Mary Edith Hancock.
Nd. Ismail Salel Ismail.
Nd. Itala Francis Xaver Itala.
Nd. Leonard Manwa Kaboboye.
Nd. Ibrahim Mohamed Kaduma.
Nd. Emanuel Kibira.
Nd. Kasmiri Yohani Komba.
Nd. Nicholaus Alfred Kuhanga.
Nd. Hindu Bori Lila.
Nd. Yahaya Bakari Lukoya.
Nd. Peter Macha.
Nd. Anne Makinda.
Nd. Abdallahman Rashid Msangi.
Nd. Jackson Wilfred Mwakimwili.
Nd. Ana Asher Namilikwa.
Nd. Phillip Ndaki.
Nd· Venance Ngula.
Nd. Saidi Ng'wanang'walu.
Nd. Robert Ng'itu
Nd. Joseph Kizurira Nyerere.
Nd. Mosi Ramadhani.
Nd. Zaituni Fadhili Selemani.
Nd. Leader Stirling.
Nd. Arnold Temu.
Nd. Crispin Tungaraza.
Nd. Ezekiel Waryuba.

## KUAHIRISHA BUNGE

**Makamu wa Rais wa Chama cha TANU:** Nd. Spika, bahati mbaya mwenzetu mmoja haonekani, sijui kama alishakata tamaa. (*Kicheko.*) Nd. Spika, sasa tumefikia mwisho wa kikao chetu hiki cha kwanza, na sasa Bunge letu limekamilika. Nawapongeza mwenzetu wote waliopita katika uchaguzi wa juzi na jana. (*Makofi.*) Nd. Spika, hapa tuko Wabunge tulioingia ndani ya Bunge hili kwa njia mbali mbali ambazo zimetajwa ndani ya Katiba yetu. Ingawa tumeingia kwa njia mbali mbali lakini wote ni Wabunge sawa na wenye haki sawa ndani ya Bunge hili. (*Makofi.*) Nd. Spika, humo ndani ya Bunge wamo wazee wetu, akina mama, na akina baba. Wamo vijana wetu, akina baba na akina mama. Wamo viongozi wa miaka mingi wa Vyama vyetu vya *AFRO-SHIRAZI PARTY* na TANU. Wamo vijana wetu wa *AFRO-SHIRAZI* na TANU. Wamo viongozi na akina mama wa U.W.T. Vile vile wamo viongozi wa Mashirika yetu yote ya TANU. Wamo Wakulima wa Kawaida na Wafanyakazi wa Kawaida. Wamo Watumishi wa Serikali, wamo wasomo wa hali ya juu sana. Juu ya haya, kuna Wanajeshi wetu, wana-TANU na Wana-*AFRO* Shupavu wakishirikiana na Ndugu zao katika mstari wa mbele wa kulijenga Taifa letu. (*Makofi.*)

Nd. Spika, hayo yote ni matokeo ya siasa yetu safi ya Ujamaa na Kujitegemea, na uongozi bora wa TANU na *AFRO-SHIRAZI PARTY.* (*Makofi.*) Matokeo haya ndiyo yanayofanya Bunge letu liwe ni shule kubwa ya siasa maana mawazo yote yanayohusu maisha ya taifa letu yanaweza kupatikana hapa. Hapa Nd. Spika, ni mkutano, au niseme makutano makubwa ya Watanzania. Bunge hili ni matokeo halisi ya ukombozi wa Watanzania, unaoendeshwa na TANU na *AFRO-SHIRAZI PARTY.* (*Makofi.*) Nd. Spika, katika nchi nyingi hapa Duniani maskini hawezi hata kugombea kuwa Mbunge, mbali kuwa Mbunge. Lakini kwa Watanzania maneno haya yamebaki sasa ni hadithi ya kuchekesha. (*Makofi.*) Huu ndiyo Ukombozi. Nd. Spika katika TANU na *AFRO-SHIRAZI PARTY* tunaamini kwamba kazi ya mapinduzi haiwezi kuendelea na kukamilika kama sehemu yoyote ya Watanzania inaachwa nyuma, hasa vijana wetu na akina mama. (*Makofi.*) kwani ukombozi wetu ni mapambano. Na mapambano ni kazi, na kazi inahitaji kila mtu.

Nd. Spika, mfano wa Taifa ni nyumba. Nyumba yenye bahati, huwa na baba, mama na watoto. Maendeleo ya nyumba yenye bahati hii, yanategemea sana tabia ya baba na mama. (*Makofi.*) Mara nyingi, mama kwa sababu ya uchungu wa watoto wake anajitahidi kila njia ili nyumbani pake pasiwe na njaa. Baba akiwa na bidii ya kazi, mama anafurahi sana, na anapata nguvu zaidi ya kufanya kazi na yeye mwenyewe. Lakini bidii ya baba haimsaidii tu mama, inasaidia zaidi kujenga tabia ya watoto. Kwa hiyo baba aliye mwema, hutangulia kwenda shamba, na mama akafuata. Baada ya kuangalia kuangalia maslahi ya vitoto pale nyumbani. Au pengine kufuatana na baba, lakini baba mwema hamwachi mama uani akisuka, na yeye anakwenda shamba peke yake. Vile vile baba mwema anapoona dalili za watoto wake kukomaa, na wanatamani kushika shoka, haraka haraka awakabidhi shoka. Maana shule ya kilimo ni kulima. Baba huyo na mama huyu, na watoto wake waliokomaa, wakilima pamoja kwa juhudi na maarifa matokeo yake ni maendeleo mazuri kwa wote. Na hasa kwa maisha ya baadaye ya watoto wao.

Nd. Spika, TANU na *AFRO-SHIRAZI PARTY* ndivyo vinavyotulea, ndivyo vinavyotufundisha. Humo ndani wamo baba zetu, mama zetu na watoto

wetu. *Letu ni moja*, kuikomboa nchi yetu. Hali hii ndiyo itakayotuwezesha kujenga zaidi na kuendeleza mapinduzi yetu. Nd. Spika, hali hii imeletwa na moja wa masikilizano makubwa yaliyomo ndani ya TANU na yaliyomo ndani ya *AFRO-SHIRAZI PARTY* na yaliyomo kati ya TANU na *AFRO-SHIRAZI PARTY* chini ya uongozi shupavu wa Nd. Mwalimu Nyerere na Nd. Aboud Jumbe. (*Makofi.*) Sisi tukiwa Kamati ya TANU na *AFRO-SHIRAZI PART*, wajibu wetu wa kwanza ni kulinda na kuendeleza umoja huu na masikilizano hayo. (*Makofi.*) Nd. Spika, letu likiendelea kuwa moja chini ya uongozi wa Vyama vyetu nguvu yetu ni kubwa. Na tutafanya makubwa. Nd. Spika kazi ya kikao hiki cha kwanza cha Bunge letu jipya ilikuwa ni kuwachagua wenzetu wakushirikiana ndani ya Bunge hili na wa kuliwakilisha Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki. Kazi hiyo tumeifanya vizuri sana, tumewapata wenzetu wana-TANU na Wana-*AFRO SHIRAZI PARTY* shupavu wa kushirikiana nao ndani ya Bunge hili. Vile vile tumewapata wana-TANU na Wana-*AFRO SHIRAZI PARTY* wenye mawazo ya kimapinduzi ambao watakao tuwakilisha katika Bunge letu la Afrika Mashariki. Wote hawa tuliwachagua kuwatakia kheri katika kazi kubwa ya kulijenga Taifa letu (*Makofi.*)

Nd. Spika, natoa salamu zangu maalum kwa akina mama wa Tanzania. (*Makofi na vifijo.*) Haya ndiyo mapinduzi tunayoyatazamia. (*Makofi.*) Nawapongeza kwa ushindi mkubwa mliofikia akina mama wa Tanzania mwaka huu. (*Makofi.*) Haya ni matokeo ya nyinyi wenyewe mama zetu kuitumia vizuri nafasi ambayo TANU na *AFRO-SHIRAZI PARTY* imetoa kwa Wana-TANU na Wana-*AFRO-SHIRAZI PARTY* bila ya ubaguzi. (*Makofi.*) Kwa kujitokeza vizuri, katika uchaguzi wa mwaka huu kama mlivyofanya, mmelisaidia Taifa kujikomboa. Mmesaidia sana kutimiza kwa vitendo siasa yetu ya usawa wa binadamu. Sasa tutajivuna kwamba katika Bunge la Tanzania tunao akina mama 17. (*Makofi.*) Ambao wamekuwa Wabunge kwa uwezo wao na uaminifu wao. (*Makofi.*) Tunao pia akina mama wawili shupavu katika Bunge la Afrika Mashariki. (*Makofi.*)

Nd. Spika, hii ni hatua ndogo sana, tukilinganisha na shabaha yetu ya kuleta usawa. Lakini huu ni mwanzo siyo mwisho. Maana wengine watafikiri kwamba huo ni mwaka wa mwanzo wa akina mama na mwisho. (*Kicheko.*) Siyo mwisho, huu ni mwanzo. (*Kicheko.*) Nd. Spika, tunajivuna kwa sababu tunajilinganisha na Mabunge ya wenzetu, hapa duniani. Tukilinganisha tuko mstari wa mbele lakini siyo kwa nambari ya akina mama waliomo humo ndani. Zaidi tunajivunia kwa ile haki, ile haki sawa ambayo TANU na *AFRO-SHIRAZI PARTY* inatoa kwa akina mama na akina baba wa Tanzania kuingia ndani ya Bunge lao. (*Makofi.*) Hata leo tunashuhudia matokeo yake.

Nd. Spika, TANU na *AFRO-SHIRAZI PARTY* itaendelea kufanya makubwa zaidi, zaidi ya haya. *A LUTA CONTINUA*. (*Makofi.*)

Nd. Spika, tunaanza kazi ya Bunge hili jipya vizuri sana. Nakupa pongezi wewe pamoja na wenzangu wote ndani ya Bunge hili. Natoa pongezi kwa Tume ya Uchaguzi na watumishi wake wote kwa kazi njema walioifanya. (*Makofi.*) Nd. Spika, natoa pongezi maalum kwa Mwenyekiti Mdogo wa TUME hiyo, Nd. Pius Msekwa. (*Makofi.*) Ambaye alishikia uongozi wa kazi ya uchaguzi wakati mwenyekiti mwenyewe yuko kwenye jimbo la uchaguzi. Nd. Pius Msekwa aliifanya kazi yake kwa moyo na uhodari mkubwa. (*Makofi.*) Nd. Spika, baada ya haya machache naomba kutoa hoja, kwamba Bunge liahirishwe mpaka tarehe 20 Januari, 1976. (*Makofi.*)

**Nd. John Malecela:** Nd. Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**Nd. Mang'enya:** Nd. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Nachukua nafasi hii kujieleza kwamba siku ya Alhamisi ulipochaguliwa nilikuwapo. Lakini zilipotoka hotuba za kukupa pongezi mimi sikuwapo kwa ajili ya shuguli nyingine; lakini papo hapo nikawa na sababu ya pili ya kuchukua nafasi hii na kujieleza kwamba nitoe shukurani zangu kwa yule Mbunge mmoja aliyeniapa kura siku ile. (*Kicheko.*) Lakini sitasema hiyo kwa sababu Nd. Makamu wa Rais wa Chama cha TANU alikwisha isemea kwa kirefu sana jana; kwa hiyo jambo hilo sitalisemea na natoa shukurani kwa Nd. Rashidi Mfaume Kawawa kwa maelezo yake jana. (*Makofi.*)

Sasa Nd. Spika naungana na wenzangu kukupa pongezi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge hili. Kama alivyosema Mheshimiwa Thabit Kombo kwamba wewe si mgeni wa shughuli hizi kwani kwa miaka kumi na moja ulizifanya katika Bunge hili. Na busara yako, hekima yake na uamuzi wako ulifanya wote tukupe heshima ile ile inayostahili Maspika wote katika Nchi za Madola. (*Makofi*). Na kusema kweli ni kwamba mimi mweyewe niko chini yako nikiwa Naibu wako; na kabla ya hapa nilikua nikimsaidia Dakta Karimjee. Kwa Dakta karimjee nilijifunza mengi lakini nasema kwa dhati nikwamba chini yako nilijifunza mengi zaidi. Kwa Kuwa ni Mwana-TANU nitasema kweli kwamba katika yote niliyojifunza kwake moja nimeshindwa na hilo namwachia Nd. Kasusura ambaye nampa pongezi kwa kuchaguliwa tena; nalo ni lile la kukaa kwenye kiti hicho kwa masaa mengi. (*Kicheko.*) Nd. Wabunge wanakumbuka kwamba mimi sikutimiza hata saa mbili. (*Kicheko.*) Kwa sababu kiti hicho kweli kina joto. (*Kicheko.*) Lakini kama ninavyosema kwamba jambo hilo sote tunakupa heko kwamba unaweza kukaa kwa masaa mengi na muda mrefu.

Sasa basi; natoa shukurani zangu kwa wale wote walioongozwa na Nd. Makamu wa Rais wa Chama cha TANU kunipa pongezi kwa kazi niliyoifanya kwenye kiti hicho kwa miaka miwili nikiwa Spika. Nasema kama nilivyosema wakati tunafunga Bunge lililopita kwamba hayo yote ikiwa tulifanikiwa ni kwa ajili ya ushirikiano wetu na uvumilivu wenu wale Wabunge waliokuwapo kwamba walinivumilia sana hasa kwenye maswali ya nyongeza. Kwa hivyo mimi nasema kwamba uvumilivu huo pamoja na ushirikiano tumpe *Chief* Adam Sapi—Spika, wetu wa sasa. (*Makofi.*) Kwani tukifanya hivyo sote tutaifanya kazi ya kiti iwe rahisi na tutazidi kuweka pale pale heshima ya Bunge letu. (*Makofi.*)

Hapa napenda kukumbusha maneno niliyoyasema juzi kwamba Bunge la Tanzania lina sifa kubwa sana katika nchi zote za Madola na hata mwaka huu

[Nd. Mang'enya]

tulipowajibu Chama cha Wabunge Nchi za Madola kwamba kwa kuwa tuna uchaguzi na ni kawaida; kwamba hatuwezi kuhudhuria au kupeleka ujumbe kwenye mkutano wa Mabunge ya Nchi za Madola; walisema tunajua hayo lakini tunasikitika sana kukosa Ujumbe wa Tanzania kwa sababu ujumbe wa Tanzania kwenye mkutano huo wa Wabunge unatakikana sana. Kwa hiyo hayo yote yamekuja kwa sababu ya sifa za Bunge hili la Tanzania. Kwa hiyo nawaomba Wabunge wenzangu wageni kwamba tushikilie vizuri. (*Makofi.*)

Sasa naendelea kutoa pongezi zangu kwa Wabunge wa zamani; hasa wale waliopita bila kupingwa. (*Kicheko.*) Narudia wito ule ule niliosema katika Bunge hili hili katika mwaka 1965; kwamba ingefa wangetupa na sisi *Seminar* ingawa na sisi tukapita siku moja bila kupingwa! (*Kicheko.*) Halafu nawapongeza Wabunge wenzangu ambao tulipata msuko suko sana hata wengine hata wengine tunataka livu ya wiki mbili tukapumzike kwa msuko suko tulioupata. Halafu nawapa pongezi wageni wote walioingia kwa kura; na wananchi walioingia kwa kura zetu hapa baada ya kupendekezwa na mashirika yetu mbali mbali. Wote nawapongeza na nawaambia kwamba sisi tupo wa zamani; tutawapa kila msaada wanaoutaka.

Sasa napenda kusema; kuunga mkono alivyosema Nd. Rashidi Mfaume Kawawa. Ninawapongeza kina mama na idadi yao imezidi wamekuwa 17 safari hii; basi nawaonya Wabunge wengine kwamba waangalie hapo! (*Kicheko.*) Bunge lililopita tulikuwa na wachache lakini palipitwa. Sasa wako 17 basi kwa hivyo muangalie. (*Kicheko.*) Nawakaribisha wakina mama—nawapa pongezi kwamba huu ni mwaka wao; na idadi hiyo inaonyesha kwamba wametimiza lengo lao la kwamba mwaka huu wakina mama waongezeke katika Bunge letu; na hilo ni jambo la kufurahisha sana. (*Makofi.*)

Nikiacha upande huo nasema kwa maoni yangu mimi binafsi kwamba ukumbi wetu leo mechanganika sana na unang'ara; hasa kwa mavazi rasmi ya kina mama na vile vile kwa vilemba. (*Kicheko.*) Mwisho nawatakia heri na fanaka wote waliomo katika Bunge hili na nawakumbusha maneno haya kwamba Ubunge ni kazi. Ahsanteni sana.

**Nd. Leader Stirling:** Nd. Spika, nakushukuru na kusema ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuunga mkono haya yaliyosemwa, kwa kifupi; kwa sababu karibu yote yameishasemwa. Hata hivyo nashukuru kupata nafasi ili kwanza nikupongeze wewe Nd. Spika, kwa kuchaguliwa tena uwe msimamizi wetu katika Bunge hili tukufu. Pamoja na hayo napenda kuwapongeza Wabunge wote wenzangu walijaribu kurudi safari hii pamoja na wageni walioingia mara ya kwanza. (*Makofi.*) Na tukisema hivyo nadhani ni haki niseme pole kwa wale wenzetu ambao hawakuwahi kurudi safari hii.

Pamoja na hayo nadhani ni vizuri niseme hivi kwa upande wao na kwa niaba ya Wabunge wenzangu waliochaguliwa juzi na jana; ni vizuri tutoe shukurani kwa Bunge hili lililotuchagua. (*Makofi.*) Ahsanteni sana. (*Makofi.*) Mwishowe Nd. Spika, napenda kukuahidi kwamba sisi Wabunge tutakuwa macho daima kuhifadhi heshima ya kiti chako kwa kufuata vizuri aumuzi wako katika shughuli zote za Bunge hili. Na zaidi ya yote nadhani naweza kusema kwamba sisi sote tuko hapa kwa kazi—kazi kubwa. Na katika kazi hii tutajitahidi daima kutekeleza maazimio ya TANU na *AFRO SHIRAZI PARTY* katika kutunga sheria na katika shughuli zote za Bunge. Kwa hiyo nakutakia wewe Nd. Spika, heri sana katika kazi yako na Wabunge wenzangu wote katika kazi hii tulioingia safari hii. (*Makofi.*)

**Nd. Mboni Cheka:** Nd. Spika, na mimi napenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuunga mkono yote yaliyokwisha semwa. Napenda pia kuchukua afasi hii kukupongeza tena Nd. Spika, kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine tena ili kuweza kuliongoza Bunge hili. Napenda pia kuchukua nafasi hii kumshukuru Nd. Makamu wa Rais wa Chama katika ushupavu wake na jitihada yake kubwa ambayo ametuonyesha wakati wote katika uongozi safi wa kuliongoza Bunge hili. (*Makofi.*) Napenda pia kuendeleza shuku ani tangu—pongezi zangu wa Nd. Wabunge wote ambao wako katika Bunge hili kwa njia mbali mbali walizopitia. Lakini pia napenda kuwapa pole wale ambao walipata misukosuko zaidi. Na sote tuliopo hapa tunatoa shukurani hiyo. Katika kumalizia Nd. Spika, napenda kuwashukuru Nd. Wabunge wote pamoja na Mtukufu Rais katika kubadilisha sura ya Bunge hili. (*Makofi.*)

Kama walivyokwishasema Ndugu walionitangulia kwamba sura ya Bunge imebadilika; na hii ni historia. Ni tumaini langu kwamba mabadiliko haya ni ya mwanzo na kwamba yataendelea mpaka itakapofikia kwamba kuna ule! (*Kicheko.*)

**Wabunge:** Usawa! (*Kicheko.*)

**Nd. Mboni Cheka:** Napemda pia Mheshimiwa Nd. Spika, kukutakia heri katika kazi ambayo umechaguliwa na Nd. Wabunge kwa kipindi cha miaka mitano inayofuata; napenda pia kuzungumza kwa niaba ya wenzangu waliochaguliwa juzi na jana pamoja na mimi mwenyewe kwamba natumaini tutashirikiana kama ilivyokuwa desturi ya Bunge hili kushirikiana katika kutekeleza shughuli za Bunge. Ahsante sana. (*Makofi.*)

(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

(*Saa 4·15 za Asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka tarehe 20 mwezi Januari, 1976*).